JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

## VITENDO VINAVYOKATAZWA NA SHERIA YA VYAMA VYA SIASA SURA 258 TOLEO LA UREKEBU LA MWAKA 2023

Chama cha siasa katika muda wote; iwe kabla, wakati na baada ya kipindi cha uchaguzi hakipaswi kufanya yafuatayo:-

i. Kuwa na malengo na madhumuni yanayopingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar au Sheria zingine za nchi;

ii. Kuunda kikundi cha ulinzi na usalama cha aina yoyote au kuwa na taasisi inayolenga kufanya majukumu ya Jeshi la Polisi au vikosi vingine vya ulinzi na usalama wa nchi;

iii. Kuratibu, kuendesha au kufadhili mafunzo yoyote ya kutumia nguvu au silaha kwa wanachama wake au kwa mtu yeyote;

iv. Kuhamasisha udini, ukabila na ukanda;

v. Kuhamasisha kuvunjika kwa Muungano wa Tanzania au kuwa na lengo la kufanya siasa upande mmoja wa muungano;

vi. Kuruhusu au kuhamasisha matumizi ya nguvu kama njia ya kufikia malengo ya kisiasa;

vii. Kuruhusu viongozi au wanachama wake kutumia maneno ya matusi, dhihaka, kashfa na uchochezi, yanayoweza kusababisha uvunjifu wa amani;

viii. Kupeperusha bendera ya chama, kufanya siasa au kufungua tawi katika maeneo ya kazi, shule, vyuo, ibada, majengo ya Serikali au Umma;

ix. Kutoa matamshi, kuandaa machapisho, kuharibu au kufanya kitendo chochote chenye dhamira ya kudhalilisha au kudhihaki bendera ya chama kingine;

x. Kufanya mikutano au maandamano bila kufuata utaratibu wa kisheria.

orpptanzania

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi -
Mtaa wa Nzuguni A
S.L.P. 2851, DODOMA

Tovuti yetu